

DIRA

Ya **Taifa**

#1



Barabara ambayo hatujawahi kuisafiria

EMMANUEL PHINEHAS MASIBAYI

DIBAJI

Kitabu hiki kinahusu utawala bora nchini Tanzania. Kimeandikwa kwa ajili ya kujaza au kuondoa kabisa bonde lilipo kati ya mifumo ya kisiasa, kiutawala na kiuchumi nchini mwetu.

Bonde hili limesababisha kuwepo kwa dhana mbalimbali za utawala bora. Kwa kuwa maendeleo ni zao la utawala bora wa mahali husika basi kuna haja ya kuwa na dhana moja shirikishi kuhusu utawala bora ili kurahisisha ushirika wa watu wote katika maendeleo.

Aidha kitabu hiki kimekusudiwa kuingiza ufahamu, ujuzi na mtizamo mpya kwa waandaa sera na wananchi kwa ujumla kuelekea dhana moja ya kitaifa katika misingi ya utawala bora.

Kusudi hili litazamiwe kama ufunguo muhimu kabisa katika kujenga uwezo mpya kwa ajili ya mabadiliko mapya ya kitabia, mitizamo na sura ya nje katika mambo yote yahasuyo utawala bora kwa maendeleo ya Taifa.

Kitabu kimeandaliwa katika namna ambayo inaashiria au kuelekeza uhusiano wa ujumla kati ya mifumo hiyo tajwa hapo juu na uwezeno wa kuiakisi katika mchakato wa kuliendeleza taifa letu kiuongozi.

Ikiwa msomaji wangu atamaliza sur azote na akaelewa kinaga ubaga kabisa juu ya dhana hii mpya ya utawala bora basi dhumuni la kitabu hiki litakuwa limefikiwa.

Nakutakia safari njema kuelekea utawala bora nchini mwetu.

MAALUMU

Kitabu kimeandikwa kuwashibisha wananchi wenye shauku kubwa ya kuona nchi yetu inaendelea.

Kwa wote wenye ndoto kuhusu mageuzi ya kisiasa, kiutawala, na kiuchumi nchini mwetu basi watarajie kupata ufahamu wa njia za kufanikisha ndoto hii kutoka kwenye kitabu hiki.

Kwa watazania wazalendo wote, kesho ya taifa letu imedhaminishwa kwetu. Kama hatutaamua kulipa dhamana ya deni hili basi vizazi vyetu vinaweza kuja kulilipa kwa machozi, jasho na damu.

Inuka leo kwa kujielimisha kuhusu milengwa mipya ya kisiasa, kiutawala na kiuchumi kwa ajili ya nchi yetu. Mambo haya matatu ni mithili ya malango ya jumba la maendeleo katika taifa letu.

Milengwa hii ndo majibu ya maombi yetu yaliyo katika wimbo wetu wa taifa